JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA KUMI

Oktoba 2023




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati alipofunga Mkutano Mkuu wa Tisa wa Lishe kwenye ukumbi wa hoteli ya Mount Meru jijini Arusha Kushoto.



Waziri Mhagama, Azindua Muongozo wa Uwekezaji Mkoa wa Manyara.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama ametoa wito kwa watendaji wa Serikali; kujipanga na kuhakikisha Muongozo wa uwekezaji kwa Mkoa Manyara unawafikia wananchi wote ili kufanya kazi kwa tija.

Kauli hiyo ameitoa Mkoani Manyara wakati wa Ufunguzi wa wiki ya Kitaifa ya Vijana tukio alilolifanya kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa jana tarehe 10/10/2023.

“Tunataka Muongozo huu uweze kutoa fursa nyingi kwa vijana ili uweze kujenga kizazi ambacho kitatatumia Muongozo huu kwa muda mrefu” alieleza.

Aliendelea kusema kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu italeta timu ya baraza la uwezeshaji kiuchumi, timu ambayo itasaidia kujenga uwezo kwenye dhana kutengeneza vitu asilia (Local content) ili kuongeza tija na kuweka mazingira wezeshi yatakayochochea wanawekezaji.

"Makapuni yaliyowekeza katika Mkoa wa Manyara yaone namna ya kutumia fedha zile zinazorudi kwa jamii, kwa kuwekeza katika vikundi vya vijana wabunifu ili kupitia muongozo wa uwekezaji usaidie kuleta tija kwa vijana na maendeleo ya Mkoa," alihimiza

Akizungumza kuhusu madhimisho ya wiki ya vijana, Mhe. Waziri Mhagama amesema ubunifu aliyouona wakati alipotembelea Mabanda, hasa uliofanywa na kijana Said Mussa wa kubuni namna ya kutengeneza taa za magari zilozoharibika na kurudisha katika muonekano mpya ni ubunifu mzuri.

"Kijana Huyu wa Kitanzania akifanikiwa kuhuisha teknolojia hiyo basi tutakuwa uwezo huko mbele kujenga viwanda vidogo vidogo vingi vya kuzalisha taa za magari nakusaidia kuongeza pato la kigeni na Kubrand Tanzania ya Mhe. Samia Kupitia Ubunifu wa Vijana," alisema.

Namshukuru sana Mhe. Mhe. Prof. Joyce L. Ndalichako na Katibu Mkuu Mhandisi Cyprian John Luhemeja kwa kuridhia kumpatia Mkopo kijana huyu ili kuhakikisha anafanya vizuri katika ugunduzi alioufanya.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi vijana ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Joyce Ndalichako amesema wiki ya vijana inalenga kutambua Mchango wa Waasisi wa Taifa Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Hayati Shekh Abeid Amani Karume.

Ameongeza kusema Maadhimisho ya wiki ya vijana Kitaifa ya Mwaka 2023 yanayofanyika Mkoani Manyara, kauli mbiu yake ni," Vijana na Ujuzi Rafiki kwa Mazingira na Maendeleo Endelevu". Maadhimisho ya vijana yanakutanisha vijana na wananchi wa Mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani ambapo vijana wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu



# Madereva wa malori watakiwa kuchukua tahadhari maambukizi ya VVU

Madereva wa magari yaendayo masafa marefu ndani ya ndani na nje Nchi wamehimizwa kuchukua tahadhari dhdi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI wakati wote wanaofanya shughuli zao za usafirishaji pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya zao ili kuanza matumizi ya dawa mapema pindi watakapogundulika kuwa na maambukizi.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga wakati akizungumza na madereva wa malori wanaoegesha malori hayo pamoja na kukagua Kituo cha Maarifa ya UKIMWI Halimashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida akiwa ameambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Afya na UKIMWI .

Mhe. Ummy amesema lengo la kufika katika kituo hicho ni kuzungumza na madereva hao akisema wako katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Kutokana na shughuli zao za masafa marefu pamoja na kukagua huduma za kiafya zinazotolewa kituoni hapo.

“Nipende kuwakumbusha na kuwasisitiza mjitokeze mpime afya zenu ili mjue mko katika hali gani, tunatambua kulingana na kazi zenu mnatembea umbali mrefu na mnaenda maeneo mengi kama mikoani na nje ya Nchi kwahiyo mko hatarini kupata maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na niwaombe mtumie kituo hiki cha Maarifa kupata elimu ya UKIMWI na magonjwa mengine ili muwe salama,” Amesema Mhe. Ummy.

Aidha Naibu Waziri huyo amewakumbusha kuendelea na matumizi ya dawa kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIWMI ili kuimarisha kinga ya mwili, kujiepusha na magonjwa nyemelezi ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi wakiwa imara kiafya huku akiisisitiza jamii kutowanyanyapaa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na badala yake kuwaonyesha upendo, kuwajali na kuwashirikisha katika maendeleo.

Aidha akisoma taarifa ya Kituo hicho mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Afya na UKIMWI Mratibu wa UKIMWI Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Dkt. Ainea Mlewa amebainisha kuwa hali ya upimaji kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Septemba 2023 jumla ya madereva wa malori waliojitokeza kupima maambukizi ya VVU ni 684 waliogundulika na maambukizi wakiwa ni 19 kati yao 15 ni wanawake wakati wanaume wakiwa ni wanne ambapo waliunganishwa katika Kliniki ya tiba na mafunzo.

“Malengo ya mradi ni kuhamasisha wananchi kupima bila uoga, kutoa ushauri, kuhamasisha upimaji wa VVU kwa hiari, kuhamasisha upimaji kwa kutumia ushawishi wa mtoa wa huduma, kutoa elimu ya UKIMWI pamoja na matibabu ya magonjwa ya zinaa, kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, kugawa kinga na elimu ya matumizi yake, elimu kwa vikundi vya WAVIU na elimu sahihi ya matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU,” Amefafanua Dkt. Mlewa.



Naibu Waziri Mhe. Khamis Hamza Akumbusha wananchi kuchukua tahadhari juu ya maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza ameiasa jamii kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI nchini kwa kuendelea kuzingatia elimu inayotolewa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ili kuunga mkono jitihada za Serikali dhidi ya mapambano hayo na kuyafikia malengo yaliyopo.

Ametoa wito huo wakati akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu alipotembelea na kujionea shughuli zinazoratibiwa na ofisi hiyo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Vijana na Wiki ya Kimataifa ya kupunguza madhara ya maafa yanayoendelea katika viwanja vya Stendi ya zamani ya mabasi Babati mkoani Manyara.

Ametoa wito huo wakati akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu alipotembelea na kujionea shughuli zinazoratibiwa na ofisi hiyo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Vijana na Wiki ya Kimataifa ya kupunguza madhara ya maafa yanayoendelea katika viwanja vya Stendi ya zamani ya mabasi Babati mkoani Manyara.Maonesho yanayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambapo yameambatana na uwepo wa maonesho mbalimbnali ya shughuli za uzalishaji, burudani, ujasiriamali na michezo iliyobeba jumbe za elimu kwa vijana katika kuipamba wiki hiyo.

Naibu Waziri huyo amesema kuwa, jamii haina budi kuendelea kujilinda na kuwalinda wengine kwa kuzingatia ushauri na elimu inayotolewa ili kuhakikisha hali ya maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI nchini ipungua na kuyafikia malengo ya kuzifikia sifuri tatu ifikapo 2030.“TACAIDS imeendelea kufanya kazi nzuri ya kuifikia jamii kwa njia

“TACAIDS imeendelea kufanya kazi nzuri ya kuifikia jamii kwa njia ya elimu, ila endeleeni kuongeza nguvu kwa vijana kwani ndilo kundi linaloongoza kwa maambukizi bila kusahau ni kundi muhimu katika uzalishaji na kujiletea maendeleo yetu, hivyo elimisheni kwa nguvu watu wabadili mitazamo yao,” alisema Mhe. Hamza

Aliongezea kuwa, Tume iendelee kutoa elimu ya matumizi sahihi ya Kondomu ili kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI hasa kwa kundi la vijana nchini.

“Endeleeni kufunga makasha ya kondomu katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu ikiwemo; kumbi za burudani, baa na nyumba za wageni lengo ni kuendelea kupunguza maambuki ya VVU na UKIMWI,” alisisitiza



## Katibu Mkuu Kiongozi Aipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa mji wa serikali

Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Dkt. Moses Kusiluka ameipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Uratibu na Usimamizi mzuri wa Ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Ametoa pongezi hizo mapema alipokuwa katika ziara maalum ya Makatibu Wakuu ya kutembelea mji wa Serikali Mtumba Dodoma ambapo alisema mafanikio ya mradi huu wa ujenzi wa Mji wa Serikali ni kukamilika kwa ukamilifu wake akitolea mfano ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa kuwa ni alama kubwa ambao utatumika kwa mambo mengi ikiwa ni pamoja na wageni kujifunza nini ambacho Tanzania imefanya.

"Tunathamini kazi yenu kubwa sana mnayofanya, kama tulivyosema awali kwenye Wasilisho, hii kazi inahitaji Uratibu kwa Sababu ni kazi ya Serikali, siyo kazi ya mmoja kuwa amemaliza na wengine kujisikia vibaya, tunashukuru kwa kutupitisha kwenye kazi kuanzia mwanzo,

tumeona juhudi kubwa za wataalamu wetu na wasimamizi lakini pia tumeona kazi kubwa iliyopo mbele na tunatambua kwamba baadhi ya wadau wanakaribia kumaliza kazi zao." Alisema Mhe. Balozi Kusiluka.

Aliendelea kusema kuwa bado kuna muda wa kutosha wa kutatua Changamoto ndogo zilizobainika katika ziara hiyo; na kusisitiza kuutazama mradi huo kwa ujumla wake kama Serikali moja, na kazi ya uratibu ikiendelea lakini pamoja na kuimarisha timu ya wataalamu wa ngazi zote katika ujenzi na kuwasikiliza, "Ni Fursa Pekee ambayo tumepewa ya kujenga Makao Makuu ya Serikali mapya na Serikali imetoa fedha nyingi kwa hivyo ni lazima sisi wataalam tufanye kazi inavyopaswa." Alisisitiza.

Alimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kutekeleza mradi huo, na kuwapa uhuru wataalam kufanya kazi ya kitaalam inavyopaswa, na kushauri wadau wengi kushiriki katika kazi hiyo pamoja na kujadili mambo ya kitaalam ili watu wengi waweze kujifunza

Kwa Upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonaz alisema swala la ushirikishwaji wa wataalam katika ujenzi wa mji wa Serikali ni swala la muhimu sana, na wadau mbalimbali wanashirikishwa kwa ajili ya kuja kuwekeza katika maeneo mbali mbali ambayo yametengwa katika mji huo wa Serikali,na majengo hayo ya Mji wa Serikali yapo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji.

## Ofisi ya Waziri Mkuu Kuendelea kushirikiana na wadau wa masuala ya lishe.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amekutana na kufanya mazungumzo na wadau wa maendeleo wa Shirika Helen Keller Tanzania ofisini kwake Jijini Dodoma.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano na wadau hao katika kuhakikisha sekta ya lishe inapewa kipaumbele ili kuwa na Taifa lenye lishe bora kuanzia ngazi ya familia.

Dkt. Yonazi amesema Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kusirikiana na wadau wa maendeleo kuhakikisha afua za lishe zinaboreshwa kwa wananchi kuhamasishwa kula vyakula vyenye virutubisho kwa kuzingatia mazingira yao yanayowazunguka pamoja na wananchi kupewa elimu ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele ili kujikinga kwa ustawi wa Taifa.

"Ipo haja ya kushirikiana pamoja tuhakikishe wananchi tunabadilisha fikra za Jamii kuhusu masuala ya lishe



Naye Mkurugenzi wa Shirika linalojishughulisha na masuala ya lishe la Helen Keller Tanzania, Dkt. Deogratius Ngoma ameeleza kwamba jukumu lao kubwa ni kujenga uelewa kwa jamii kuhusu vyakula hatarishi vinavyosababisha magonjwa yasiyoambukiza.

.

Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz